Editon Consortium Journal of Kiswahili [ISSN: 2663 -9289]

Issue no: 01 | Vol no: 07 | September 2026: 85-101

# Ubabedume na Dhiki za Mwanamume katika Riwaya za Kiswahili za Waandishi Wanawake

**Wasike Moses** [1]
**Wafula Magdaline** [2]
**Mosol Kandagor** [3]

**(1.2.3)** Moi University, Kenya.
Main author's email: mmwasike@gmail.com

**Article History**
Received: **2026.07.18**
Accepted: **2026.08.10**
Published: **2026.09.04**

**Cite this article in APA**
Wasike, M., Wafula, M., & Kandagor, M. (2026). Ubabedume na dhiki za mwanamume katika riwaya za Kiswahili za waandishi wanawake. *Editon consortium journal of kiswahili, 7*(1), 85–101. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v7i1.748

**Ikisiri**
Tafiti nyingi kuhusu ubabedume katika fasihi ya Kiswahili zimejikita katika athari zake kwa wanawake, huku gharama zake kwa wanaume wenyewe zikipewa uzito mdogo. Makala hii inachunguza namna ubabedume inavyokuwa chanzo cha dhiki kwa wahusika wa kiume katika riwaya teule za Kiswahili zilizoandikwa na waandishi wanawake. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Ubabedume ya Connell (1995) na ulitumia mkabala wa kimaelezo wenye mwelekeo wa uchanganuzi wa yaliyomo ya kifasihi. Data ilikusanywa kutoka *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2019) na *Penzi la Damu* (Manyanza, 2017), zilizoteuliwa kimakusudi, kwa kuchanganua matukio, mazungumzo na mienendo ya wahusika wa kiume kwa kuzingatia uhusiano kati ya matarajio ya uanaume na dhiki wanazopitia. Matokeo yanaonyesha kuwa dhiki ya wanaume katika riwaya hizi haitokani tu na kushindwa kutimiza matarajio ya ubabedume, bali pia na gharama za kuyatimiza. Ulinganishi unaonyesha kuwa, licha ya tofauti za mazingira, kuna kinzani ya msingi ambapo sifa zinazotumiwa kujenga na kuthibitisha uanaume wakati huohuo zinaweza kuuporomosha ustawi wa mwanaume. Makala inahitimisha kuwa ubabedume unaweza kuwa mzigo kwa wanaume wenyewe pale matarajio ya uanaume yanapowalazimisha kuthibitisha nguvu, mamlaka na uwezo wao kwa gharama ya afya, ustawi na mahusiano yao. Kwa hivyo, makala inapendekeza kuimarishwa kwa mijadala na tafiti kuhusu miundo mbadala ya uanaume inayosisitiza uwajibikaji, ushirikiano, mawasiliano, usawa wa kijinsia na kuthamini afya ya kimwili na kiakili ya wanaume. Makala hii inapanua mjadala wa ubabedume katika fasihi ya Kiswahili kwa kuonyesha kuwa wanaume wanaweza kuwa watendaji wa mfumo wa ubabedume na wakati huohuo kuwa wahanga wa gharama zake za kimwili, kiakili, kiuchumi na kijamii.

**Maneno Muhimu**: Afya ya akili, dhiki za mwanamume, riwaya za Kiswahili, ubabedume, waandishi wanawake.

Editon OPEN ACCESS

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

**UTANGULIZI**

Mijadala kuhusu ubabedume katika tafiti za jinsia na fasihi, hususan fasihi ya Kiswahili, imekuwa ikizingatia zaidi athari za mfumo huo kwa wanawake, huku athari zake kwa wanaume zikipewa uangalizi mdogo. Kwa kiasi kikubwa, msisitizo umewekwa katika namna mfumo huu unavyowapa wanaume mamlaka na upendeleo huku ukiwaweka wanawake katika nafasi za chini kijamii, kiuchumi na kisiasa. Kwa mujibu wa Connell (1995), ubabedume (*hegemonic masculinity*) ni aina ya uanaume inayopewa hadhi ya juu kuliko aina nyingine za uanaume na hivyo kuhalalisha mahusiano ya nguvu katika jamii. Mfumo huu hujengwa kupitia matarajio ya kijamii yanayomtaka mwanaume kuwa mwenye mamlaka, jasiri, mshindani, mwenye kujitegemea, mwenye uwezo wa kudhibiti mazingira yake na asiyeonyesha udhaifu wa kihisia. Kupitia taasisi kama familia, elimu, dini na utamaduni, wanaume hufunzwa kufuata viwango hivi ili watambulike kama "wanaume halisi" (Connell & Messerschmidt, 2005). Kwa hiyo, pamoja na kuchunguza namna ubabedume unavyowaathiri wanawake, ni muhimu pia kuchunguza gharama ambazo mfumo huo unaweza kuwabebesha wanaume wenyewe.

Kwa muda mrefu, tafiti za kifeministi zimeonyesha namna ubabedume unavyochangia ukandamizaji wa wanawake na kuendeleza usawa usio sawa wa kijinsia (Millett, 1970; Lerner, 1986; Walby, 1990; hooks, 2000). Hata hivyo, wataalamu wa tafiti za uanaume wamebainisha kuwa pamoja na manufaa ambayo baadhi ya wanaume huyapata ndani ya mfumo huo, matarajio ya ubabedume yanaweza pia kuwa chanzo cha dhiki kwa wanaume wenyewe. Katika makala hii, dhiki za mwanamume zinarejelea hali za kisaikolojia, kimwili, kijamii, kifamilia, kiuchumi na kihisia zinazoweza kuwakabili wanaume kutokana na shinikizo la kutimiza au kudumisha matarajio ya ubabedume. Kimmel (2008) anaeleza kuwa matarajio yanayomtaka mwanaume awe jasiri, mwenye mafanikio, mwenye kujitegemea na asiyeonyesha hisia yanaweza kumweka katika mazingira ya dhiki za kimwili, kihisia na kijamii. Vivyo hivyo, Messner (1997) anasema kuwa wanaume wengi hulazimika kuishi kwa kuzingatia viwango vya uanaume vinavyoweza kuwa vigumu kuvifikia, jambo linaloweza kusababisha migogoro ya ndani, msongo wa mawazo na tabia za kujidhuru. Kuchunguza dhiki hizi ni muhimu kwa sababu kunasaidia kuonyesha sura mbili za ubabedume: mfumo unaoweza kuwapa baadhi ya wanaume mamlaka, lakini wakati huo huo ukawaweka chini ya shinikizo la kutimiza viwango vya uanaume vinavyoweza kuwa na madhara kwa ustawi wao.

Katika muktadha wa Kiafrika, matarajio ya ubabedume mara nyingi huhusishwa na uwezo wa mwanaume kuwa mtoa huduma, kichwa cha familia, mwenye mamlaka na mlinzi wa familia. Matarajio haya yanaweza kumweka mwanaume katika shinikizo la kuhakikisha ustawi wa kiuchumi na kijamii wa familia yake. Silberschmidt (2001), katika utafiti wake uliohusisha jamii za Kisii nchini Kenya na Dar es Salaam nchini Tanzania, anaonyesha kwamba ukosefu wa ajira au kipato cha chini unaweza kuwazuia wanaume kutimiza majukumu yanayohusishwa na kuwa kichwa cha familia na mtafutaji wa riziki, hali inayoweza kuathiri hadhi yao ya kijamii, utambulisho na kujithamini. Aidha, Stoebenau na wenzake (2023) wanaonyesha kuwa katika miktadha mbalimbali ya Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, matarajio ya mwanaume kuwa mtoa huduma yana uhusiano na matarajio ya kuwa na mamlaka na uwezo wa kufanya maamuzi katika familia na mahusiano. Mifano hii inaonyesha kuwa matarajio ya ubabedume katika mazingira ya Kiafrika hayawezi kutenganishwa na hali za kiuchumi, kifamilia na kijamii zinazowakabili wanaume. Kwa hivyo, kushindwa kutimiza matarajio haya kunaweza kusababisha hisia za kushindwa, kupoteza hadhi ya kijamii, migogoro ya kifamilia na changamoto za kisaikolojia.

Fasihi, kama kioo cha jamii, imeendelea kuakisi mahusiano ya kijinsia na changamoto zinazotokana na mifumo ya kijamii inayounda mahusiano hayo. Kupitia wahusika, migogoro na matukio mbalimbali, waandishi huibua namna matarajio ya kijamii yanavyounda maisha ya wanaume na wanawake. Katika fasihi ya Kiswahili, masuala ya jinsia, hadhi ya mwanamke na athari za mifumo ya kijamii yenye mwelekeo wa ubabedume yamejadiliwa na watafiti mbalimbali. Kwa mfano, Bertoncini-Zúbková (1996) anaonyesha namna wanawake wanavyowasilishwa katika fasihi ya Kiswahili, hususan katika nafasi zinazohusishwa na unyanyasaji, udhibiti na ukosefu wa usawa wa kijinsia. Vilevile, Topan (2004) anachunguza mabadiliko katika uwakilishi wa hadhi ya mwanamke katika fasihi ya Kiswahili, akionyesha namna kazi za kifasihi zinavyohusiana na mitazamo ya kijamii kuhusu nafasi ya mwanamke. Osore (2015) pia amechanganua ujenzi wa uke na uanaume katika riwaya za Euphrase Kezilahabi na Said Ahmed Mohamed, akionyesha namna dhana za kijinsia zinavyojengwa na kuwasilishwa kifasihi.

Hata hivyo, mwelekeo wa tafiti hizi unaonyesha kwamba suala la jinsia katika fasihi ya Kiswahili limekuwa likijadiliwa kwa kiasi kikubwa kupitia nafasi, hadhi na ukandamizaji wa wahusika wanawake. Hali hii inaonekana pia katika kazi za Bertoncini-Zúbková (1996) na Topan (2004), ambazo zimeweka mkazo mkubwa katika uwakilishi na hadhi ya mwanamke katika fasihi ya Kiswahili. Ingawa tafiti zimeanza kuzingatia uanaume, bado kuna nafasi ya kuchunguza kwa kina namna mifumo ya ubabedume inavyoweza kuwaathiri wanaume wenyewe. Kwa mfano, Kweyu (2007), katika uchanganuzi *wa Rosa Mistika na Kichwamaji*, anaonyesha kuwa ingawa masuala ya ubabedume na uanaume yanajitokeza katika riwaya hizo, uhakiki uliotangulia haukuwa umehusisha kwa kina masuala hayo na masaibu ya wahusika wakuu. Vivyo hivyo, Onyango na Musa (2016) walipochunguza uanaume katika *Nyota ya Rehema*, walibainisha umuhimu wa kuichunguza dhana ya masculinities licha ya kwamba uhakiki wa awali ulikuwa umeelekeza zaidi katika masuala kama hatima na mapambano ya kitabaka. Kwa msingi huo, bado kuna haja ya kuchunguza namna matarajio na kanuni za ubabedume yanavyoweza kuwa chanzo cha shinikizo, migogoro na changamoto katika maisha ya wahusika wanaume katika riwaya za Kiswahili.

Waandishi wanawake wa Kiswahili wameendelea kuibua changamoto zinazowakabili wahusika wa kiume ndani ya mfumo wa ubabedume. Kupitia wahusika wao, wanaonyesha jinsi matarajio ya kuwa mwanaume jasiri, mwenye mamlaka, mtoa huduma na asiyeonyesha udhaifu yanavyoweza kusababisha madhara mbalimbali kama kudhoofika kwa afya ya kimwili, matatizo ya afya ya akili, kuhasirika kifedha, kuvurugika kwa mahusiano, upweke, kifungo, majeraha na hata vifo. Hata hivyo, mifumo hii ya dhiki bado haijachunguzwa kwa kina katika uhakiki wa riwaya za Kiswahili, ambao umeendelea kuangazia zaidi nafasi ya mwanamke ndani ya mfumo dume. Kwa msingi huo, makala hii inachunguza jinsi ubabedume unavyokuwa chanzo cha dhiki kwa wahusika wa kiume katika riwaya teule za Kiswahili zilizoandikwa na waandishi wanawake.

Makala inabainisha namna matarajio ya mamlaka na udhibiti, kujitegemea na kuwa mtoa huduma, uthubutu na ukakamavu, ukandamizaji wa kihisia, pamoja na ushindani na utawala katika mahusiano ya kijinsia yanavyohusishwa na kudhoofika kwa afya, matatizo ya kisaikolojia, hasara za kiuchumi, kuvurugika kwa mahusiano, upweke, kifungo, kuhatarisha maisha na vifo vya wahusika wa kiume. Kwa kutumia Nadharia ya Ubabedume ya Connell (1995), makala hii inachangia kupanua mjadala wa fasihi na jinsia kwa kuonyesha kuwa ubabedume hauwaathiri wanawake pekee bali pia unaweza kuwa chanzo cha mateso na dhiki kwa wanaume wanaotarajiwa kuudumisha.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Utafiti kuhusu uanaume na ubabedume umejikita katika kuelewa namna uanaume unavyojengwa na kuendelezwa kupitia taratibu za kijamii, kitamaduni na kihistoria. Connell (1995) anaeleza kuwa uanaume si hali ya kimaumbile pekee, bali ni zao la mahusiano ya kijamii na kijinsia yanayobadilika kulingana na mazingira. Katika mtazamo huu, ubabedume hujenga na kuhalalisha aina fulani ya uanaume inayohusishwa na mamlaka, udhibiti, ushindani, uthubutu, kujitegemea na uwezo wa kustahimili changamoto. Connell na Messerschmidt (2005) walipanua mjadala huu kwa kusisitiza kuwa ubabedume si sifa moja inayoshikiliwa na wanaume wote, bali ni mfumo wa mahusiano unaobadilika kulingana na mazingira ya kijamii. Kwa mtazamo huu, baadhi ya wanaume wanaweza kunufaika na nafasi za mamlaka zinazotokana na ubabedume, huku wengine wakibanwa na matarajio ya kutimiza viwango vinavyotambulika kuwa vya "uanaume halisi."

Mjadala huu umeendelezwa na watafiti waliochunguza gharama za kijamii na kisaikolojia za matarajio ya uanaume. Kimmel (2008) anaeleza kuwa uanaume huhitaji kuthibitishwa mara kwa mara mbele ya jamii na wanaume wenzao, hali inayoweza kumweka mwanaume katika shinikizo la kuonyesha nguvu, mafanikio, uwezo na udhibiti. Kwa upande mwingine, Pleck (1995), kupitia dhana ya *gender role strain*, anaonyesha kuwa matarajio ya kijinsia yanaweza kumweka mwanaume katika hali ya mkazo pale anaposhindwa au kutotaka kutimiza majukumu yanayohusishwa na uanaume. O'Neil (2008), kupitia Nadharia ya Migogoro ya Majukumu ya Kijinsia (*Gender Role Conflict Theory*), anaendeleza hoja hii kwa kuonyesha kuwa matarajio magumu ya kijinsia yanaweza kuhusishwa na matatizo katika mahusiano, afya ya akili na ustawi wa mwanaume. Courtenay (2000) naye anaonyesha kuwa kanuni za uanaume zinaweza kuathiri afya ya wanaume kwa kuwahimiza kuonyesha kutokuwa na udhaifu, kujitegemea kupita kiasi na kushiriki katika tabia hatarishi.

Hata hivyo, mitazamo hii ya jumla inahitaji kuchukuliwa kwa tahadhari inapohamishiwa katika mazingira ya Kiafrika kwa sababu uanaume hujengwa ndani ya historia, uchumi, utamaduni na mahusiano mahususi ya jamii. Katika muktadha wa Afrika, matarajio ya mwanaume kuwa mtoa huduma na mwenye mamlaka katika familia yamehusishwa kwa karibu na ujenzi wa utambulisho wa kiume. Stoebenau na wenzake (2023), katika utafiti wao wa Uganda, wanaonyesha kuwa matarajio ya mwanaume kuwa mtoa huduma wa familia yanaambatana na matarajio ya mamlaka, udhibiti wa maamuzi na majukumu maalumu katika mahusiano. Utafiti wao unaonyesha pia kuwa jukumu la mwanaume kama mtoa huduma ni msingi muhimu wa ujenzi wa uanaume katika mazingira mengi ya Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Hivyo, kushindwa kutimiza jukumu la kiuchumi kunaweza kuwa si tatizo la kifedha pekee, bali pia changamoto kwa utambulisho na hadhi ya mwanaume.

Hoja hii inaungwa mkono na Ezeugwu na Ojedokun (2020), ambao wanajadili uhusiano kati ya kanuni za uanaume na afya ya akili ya wanaume barani Afrika. Wanaonyesha kuwa ujifunzaji na ujanibishaji wa kanuni zinazomtaka mwanaume kuwa jasiri, mwenye nguvu, asiyeonyesha udhaifu na anayepaswa kukabiliana na matatizo bila kuomba msaada unaweza kuwafanya wanaume kuficha changamoto zao za kihisia na kuchelewa kutafuta msaada. Kwa mujibu wao, kanuni hizo zinaweza kuhusishwa na upweke, msongo, wasiwasi, unyogovu na tabia hatarishi. Utafiti huu ni muhimu kwa makala hii kwa sababu unaonyesha kwamba matarajio ya uanaume yanaweza kuwa na matokeo yanayompata mwanaume mwenyewe, badala ya kumwezesha tu kutawala wengine.

Katika muktadha wa Kenya, utafiti wa Ranjbar na wenzake (2021) kuhusu wanaume vijana wa Kenya unaonyesha uhusiano kati ya *gender role strain*, ufuasi wa kanuni za uanaume na dhiki ya kisaikolojia. Utafiti huo, uliohusisha wanaume vijana 391 nchini Kenya, ulibaini uhusiano kati ya ufuasi wa baadhi ya kanuni za uanaume na dalili za wasiwasi, unyogovu na dhiki ya kisaikolojia. Matokeo haya yanaimarisha hoja kwamba kanuni za uanaume zinaweza kuwa na madhara kwa ustawi wa wanaume wenyewe. Aidha, utafiti wa hivi karibuni kuhusu wavulana nchini Kenya unaonyesha kuwa matarajio mapya ya kijamii yanayohusishwa na kuwa mwanaume yanaweza kuambatana na aibu, ukimya, shinikizo la rika na kujihusisha na tabia hatarishi.

Katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili, mjadala wa uanaume umeanza kuonekana katika tafiti mbalimbali, ingawa umeendelea kuwa mdogo ukilinganishwa na tafiti zinazohusu wanawake na ukandamizaji wao katika mifumo ya kijinsia. Onyango (2007), kwa mfano, alichunguza uanaume katika fasihi ya watoto ya Kiswahili nchini Kenya na kuonyesha namna masuala ya kimwili, kijamii, kiuchumi na kisiasa yanavyohusika katika ujenzi wa uanaume. Utafiti huo unaonyesha pia kwamba itikadi na mahusiano ya mamlaka yanayohusishwa na uanaume huanza kujengwa tangu utotoni.

Kweyu (2007) alichunguza ubabedume na uanaume katika *Rosa Mistika* na *Kichwamaji* za Euphrase Kezilahabi. Utafiti wake ni muhimu zaidi kwa makala hii kwa sababu ulipendekeza kwamba wahusika wakuu katika riwaya hizo wanaweza kueleweka kama wahanga wa itikadi za ubabedume na uanaume. Kweyu anaonyesha kuwa ingawa masuala ya ubabedume na uanaume yanajitokeza katika riwaya hizo, uhakiki uliotangulia haukuwa umehusisha kwa kina itikadi hizo na masaibu ya wahusika wakuu. Hivyo, utafiti wa Kweyu unaonyesha kwamba uchanganuzi wa uanaume unaweza kuvuka mtazamo unaomwona mwanaume kama mtendaji wa mamlaka pekee na badala yake kumchunguza pia kama mhusika anayeweza kuathiriwa na mfumo wa kijinsia.

Osore (2015) pia alichunguza ujenzi wa uke na uanaume katika riwaya za Euphrase Kezilahabi na Said Ahmed Mohamed. Utafiti huo ulilenga namna waandishi hao wanavyowasilisha taswira za wasichana, wavulana, wanawake na wanaume, na ulitumia Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Diskosi kuchunguza maana za kijamii, kitamaduni na kiitikadi zinazojengwa kupitia usawiri huo. Utafiti huu unaonyesha kwamba uanaume tayari umeanza kuchukuliwa kama eneo halali la uhakiki wa fasihi ya Kiswahili, lakini haujajikita katika namna matarajio ya ubabedume yanavyoweza kuzalisha aina mbalimbali za dhiki kwa wahusika wa kiume.

Utafiti wa hivi karibuni umeendelea kupanua mwelekeo huu. Janvan (2023) alichunguza ukandamizaji wa jinsia ya kiume katika *Njozi Yapata Mtenzi* na *Nguu za Jadi*. Utafiti huo ulilenga kubainisha makundi yanayokandamiza jinsia ya kiume, athari za

ukandamizaji huo na mikakati inayotumiwa na wanaume katika kupigania ukombozi wao. Matokeo yake yanaonyesha kuwa wanaume katika *Nguu za Jadi* wanawakilishwa kwa namna mbili: baadhi yao hutumia ubabe wao kuwanyanyasa wanaume wengine wasio wababe, huku wengine wakiwakilisha aina mpya ya uanaume inayojitenga na baadhi ya sifa za ubabedume. Utafiti huu ni muhimu kwa makala ya sasa kwa sababu unathibitisha kuwa *Nguu za Jadi* tayari imechunguzwa kwa mtazamo wa ukandamizaji wa jinsia ya kiume. Hata hivyo, msisitizo wa Janvan ni ukandamizaji, makundi ya wakandamizaji na mikakati ya ukombozi; haujajikita katika uchanganuzi wa kina wa namna matarajio ya ubabedume yanavyohusishwa na afya ya kimwili, afya ya akili, matatizo ya kifedha, kuvurugika kwa mahusiano, kuhatarisha maisha na vifo vya wahusika wa kiume.

Vilevile, Kiema na wenzake (2025) wamechunguza moja kwa moja changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume katika *Nguu za Jadi*. Utafiti wao unaongozwa na Nadharia ya Uhalisia na unaangazia changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume, huku ukisisitiza kwamba tafiti nyingi za awali zimeelekea zaidi katika dhuluma zinazowakumba wanawake. Utafiti huu unaifanya hoja ya pengo kuwa pana zaidi kuwa haiwezi tena kuwa "wahusika wa kiume katika *Nguu za Jadi* hawajafanyiwa utafiti." Badala yake, pengo linapaswa kutafutwa katika aina ya swali linaloulizwa, dhana inayotumika na namna athari hizo zinavyounganishwa na matarajio ya ubabedume.

Kwa upande wa *Penzi la Damu*, tafiti zimeanza pia kulichunguza katika masuala yanayohusiana na mahusiano na afya ya akili. Maulid (2025), kwa mfano, amechunguza viashiria vya matatizo ya afya ya akili katika maisha ya ndoa kwa kutumia *Mungu Hakopeshwi* na *Penzi la Damu*. Utafiti huo unaonyesha namna matatizo ya ndoa yanavyoweza kuhusishwa na changamoto za afya ya akili katika riwaya hizo. Hata hivyo, uchanganuzi huo umejikita katika viashiria vya matatizo ya afya ya akili katika ndoa kwa mtazamo wa Saiko-Changanuzi, badala ya kuchunguza namna matarajio ya ubabedume yanavyoweza kuwa chanzo au kichocheo cha dhiki hizo kwa wahusika wa kiume.

Kwa jumla, mapitio haya yanaonyesha mwelekeo wa hatua tatu katika tafiti zilizopo. Kwanza, tafiti za kinadharia zimeonyesha kuwa uanaume na ubabedume ni miundo ya kijamii inayoweka matarajio na masharti kwa wanaume (Connell, 1995; Connell & Messerschmidt, 2005; Pleck, 1995). Pili, tafiti za Kiafrika na za Kenya zimeonyesha kwamba matarajio ya kuwa mtoa huduma, mwenye mamlaka, mwenye nguvu na asiyeonyesha udhaifu yanaweza kuwa na athari kwa ustawi na afya ya wanaume (Ezeugwu & Ojedokun, 2020; Ranjbar na wenzake, 2021; Stoebenau na wenzake, 2023). Tatu, tafiti za fasihi ya Kiswahili zimeanza kuchunguza ujenzi wa uanaume, ubabedume na ukandamizaji wa wahusika wa kiume, wakiwamo wahusika katika *Nguu za Jadi* (Onyango, 2007; Kweyu, 2007; Osore, 2015; Janvan, 2023; Kiema na wenzake, 2025).

Hata hivyo, tafiti hizi hazijaunganishwa kwa namna ya kutosha katika uchanganuzi unaochunguza matarajio ya ubabedume kama chanzo cha dhiki mbalimbali zinazowakumba wahusika wa kiume katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na wanawake. Janvan (2023) amezingatia ukandamizaji wa jinsia ya kiume katika *Nguu za Jadi*, huku Kiema na wenzake (2025) wakilenga changamoto za mhusika wa kiume katika riwaya hiyo. Kwa upande mwingine, Maulid (2025) amezingatia matatizo ya afya ya akili katika ndoa kwa kutumia *Penzi la Damu*, lakini si kwa kulichanganua kupitia dhana ya ubabedume na matarajio ya kijinsia kwa wahusika wa kiume. Kwa hiyo, pengo linalojitokeza si ukosefu wa tafiti kuhusu wanaume, bali ni ukosefu wa uchanganuzi jumuishi unaounganisha matarajio ya ubabedume na aina mbalimbali za dhiki za wahusika wa kiume katika riwaya hizi mbili.

Makala hii inalenga kuziba pengo hilo kwa kuchunguza namna ubabedume unavyohusishwa na kudhoofika kwa afya ya kimwili, matatizo ya afya ya akili, hasara au matatizo ya kifedha, kuvurugika kwa mahusiano na kuhatarisha maisha ya wahusika wa kiume katika *Nguu za Jadi* na *Penzi la Damu*. Kwa kufanya hivyo, makala inapanua mjadala wa fasihi ya Kiswahili kutoka kumtazama mwanaume hasa kama mtendaji au mnufaika wa mamlaka ya mfumo dume hadi kumchunguza pia kama mhusika anayeweza kubanwa, kuathiriwa na hata kudhurika kutokana na matarajio ya mfumo huo.

**Msingi wa Kinadharia**

Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Ubabedume inayohusishwa na Connell (1995), hasa dhana ya ubabedume au uanaume tawala. Nadharia hii inaeleza kuwa uanaume si hali ya kimaumbile pekee, bali ni ujenzi wa kijamii unaozalishwa na kuendelezwa kupitia mahusiano ya kijinsia, kijamii, kiuchumi na kitamaduni. Kwa mujibu wa Connell (1995), katika jamii hujitokeza

aina mbalimbali za uanaume ambazo hazina hadhi sawa. Aina moja inaweza kupewa hadhi na mamlaka zaidi kuliko nyingine na kutumika kama kiwango kinachotambulisha uanaume unaokubalika katika jamii. Connell anatofautisha miongoni mwa aina hizo uanaume tawala au ubabedume (*hegemonic masculinity*), uanaume shiriki (*complicit masculinity*), uanaume duni (*subordinated masculinity*) na uanaume pembezoni (*marginalized masculinity*).

Kwa mtazamo wa Connell (1995), uanaume tawala hujengwa kupitia mazoea na matarajio yanayomfanya mwanaume kuonekana kuwa na mamlaka, nguvu, uwezo wa kufanya maamuzi, kujitegemea na kustahimili changamoto. Hata hivyo, si lazima kila mwanaume awe na sifa hizo kwa kiwango cha juu ili mfumo wa ubabedume uwepo. Muhimu ni kwamba sifa hizo hutumika kama kiwango cha kijamii kinachofafanua uanaume unaoheshimiwa na unaokubalika. Connell na Messerschmidt (2005) wanaendeleza hoja hii kwa kusisitiza kwamba uanaume tawala ni dhana inayobadilika kulingana na mazingira ya kijamii na kihistoria. Kwa hiyo, matarajio ya uanaume yanapaswa kuchunguzwa katika mazingira mahususi ambamo wahusika wanaishi.

Katika makala hii, nadharia hii haijatumika kuchunguza tu namna wanaume wanavyonufaika na mamlaka ya mfumo wa ubabedume, bali pia namna matarajio ya mfumo huo yanavyoweza kuwabana na kuwazalishia dhiki. Kwa msingi huo, vipengele sita vya kinadharia vimetumika kama vigezo vya uchanganuzi: (i) mamlaka na udhibiti, (ii) kujitegemea na jukumu la uanaume kama mtoa huduma, (iii) uthubutu na ukakamavu, (iv) ukandamizaji wa kihisia, (v) ushindani na mafanikio, na (vi) utawala katika mahusiano ya kijinsia. Vipengele hivi vitahusishwa na aina mbalimbali za dhiki zinazowakumba wahusika wa kiume katika riwaya teule.

**Mamlaka na Udhibiti**

Mamlaka na udhibiti ni kipengele muhimu cha uanaume tawala kwa sababu mfumo wa ubabedume huhusisha mwanaume na uwezo wa kufanya maamuzi, kuongoza wengine na kudhibiti mazingira yake. Kwa mujibu wa Connell (1995), uanaume tawala hujengwa ndani ya mahusiano ya mamlaka na jinsia. Katika uchanganuzi huu, kipengele hiki kimetumika kubainisha namna wahusika wa kiume wanavyotarajiwa kuwa viongozi, kufanya maamuzi, kudhibiti familia au mahusiano na kudumisha hadhi yao. Uchanganuzi umeangalia pia hali ambapo mhusika anaposhindwa kutawala au kupoteza mamlaka hukumbwa na migogoro, fedheha, kuvurugika kwa mahusiano, kifungo, au dhiki ya kisaikolojia.

**Kujitegemea na Jukumu la Mtoa Huduma**

Kujitegemea na uwezo wa kumudu mahitaji ya familia ni miongoni mwa matarajio yanayohusishwa na uanaume katika mazingira mengi ya kijamii. Mwanaume anayetarajiwa kuwa mtoa huduma anatakiwa kuwa na uwezo wa kupata kipato, kutunza familia na kutatua matatizo bila kutegemea wengine. Katika makala hii, kipengele hiki kimetumika kuchanganua namna shinikizo la kuwa mtoa huduma na kujitegemea linavyoweza kuhusishwa na hasara za kifedha, kushindwa kiuchumi, migogoro ya kifamilia, kupoteza hadhi na hisia za kushindwa. Hivyo, matatizo ya kiuchumi ya wahusika yamechanganuliwa si kama matukio ya kifedha pekee, bali pia kama matokeo yanayoweza kuhusishwa na matarajio ya kijamii kuhusu uanaume.

**Uthubutu na Ukakamavu**

Uthubutu na ukakamavu vinahusishwa na matarajio kwamba mwanaume anapaswa kuwa jasiri, mwenye nguvu na mwenye uwezo wa kukabiliana na changamoto bila kuonekana dhaifu. Katika uchanganuzi huu, kipengele hiki kimetumika kuchunguza matukio ambayo wahusika wa kiume hulazimika kuonyesha nguvu, kupambana na changamoto au kukataa kuonekana kuwa waoga au wanyonge. Utafiti umeangalia pia namna msukumo huo wa kuthibitisha ukakamavu unavyoweza kuwafanya wahusika kufanya maamuzi hatarishi, kuingia katika migogoro, kutumia nguvu, kuhatarisha maisha yao au ya wengine, na hatimaye kukumbwa na majeraha au vifo.

**Ukandamizaji wa Kihisia**

Ukandamizaji wa kihisia unahusu matarajio kwamba mwanaume hapaswi kuonyesha udhaifu, kulia, kuomba msaada au kueleza wazi hisia zake. Ingawa Connell (1995) haijengi kipengele hiki kama orodha ya sifa binafsi za mwanaume, kinaweza kueleweka kutokana na namna uanaume tawala unavyohusishwa na nguvu, udhibiti na kukataa nafasi za udhaifu. Katika makala hii, kipengele hiki kimetumika kuchanganua namna wahusika wanavyoficha huzuni, hofu, maumivu au mahitaji ya msaada kwa sababu ya matarajio ya kijamii kuhusu uanaume. Uchanganuzi umeonyesha jinsi ukandamizaji huo wa kihisia unavyoweza kuhusishwa na upweke, migogoro ya mahusiano, matatizo ya afya ya akili, kujitenga kijamii na kushindwa kutafuta msaada.

**Ushindani na Mafanikio**

Ushindani ni kipengele kingine kinachohusishwa na uanaume tawala, ambapo mwanaume hutakiwa kuonyesha uwezo, mafanikio, nguvu na uwezo wa kuwazidi au kuwalinganisha wanaume wengine. Katika makala hii, kipengele hiki kimetumika kuchanganua namna wahusika wanavyolazimika kuthibitisha uwezo wao katika masuala ya kiuchumi, kijamii, kimahusiano au kimamlaka. Utafiti umeangalia namna shinikizo la kufanikiwa au kutokubali kushindwa linavyoweza kusababisha migogoro, maamuzi yasiyo na tahadhari, hasara za kifedha, kuvurugika kwa mahusiano au kuhatarisha maisha.

**Utawala katika Mahusiano ya Kijinsia**

Utawala katika mahusiano ya kijinsia unahusu matarajio kwamba mwanaume anapaswa kuwa na nafasi ya juu ya mamlaka katika mahusiano na wanawake. Kipengele hiki kinatokana na msisitizo wa Connell (1995) kwamba uanaume tawala hujengwa ndani ya mahusiano ya kijinsia na huweza kuhusishwa na uendelezaji wa mamlaka ya wanaume dhidi ya wanawake. Katika uchanganuzi huu, kipengele hiki kimetumika kuchunguza namna wahusika wa kiume wanavyotumia au kutafuta mamlaka katika mahusiano yao na wanawake, na namna kupoteza mamlaka hiyo kunavyoweza kuhusishwa na migogoro, wivu, vurugu, kuvurugika kwa mahusiano, matatizo ya kisaikolojia au tabia za kuhatarisha maisha.

Kwa msingi wa vipengele hivi, makala hii inachukulia kwamba dhiki za wahusika wa kiume haziwezi kueleweka bila kuchunguza matarajio ya kijamii yanayounda uanaume wao. Kwa mfano, mwanaume anayeshindwa kutimiza wajibu wa kuwa mtoa huduma anaweza kupata hasara ya kifedha na kupoteza hadhi; anayelazimika kuthibitisha ukakamavu anaweza kufanya vitendo vya kuhatarisha maisha; na anayezuiwa kuonyesha hisia anaweza kujikuta katika upweke, migogoro au matatizo ya afya ya akili. Kwa hiyo, uhusiano kati ya kipengele cha ubabedume na dhiki utazingatiwa katika mnyororo wa *matarajio ya kijamii → jitihada za kuyatimiza au kuyadumisha → kushindwa, mgongano au shinikizo → dhiki kwa mhusika wa kiume*.

Kwa jumla, Nadharia ya Ubabedume ilifaa kwa makala hii kwa sababu iliwezesha kuchunguza ubabedume kwa mtazamo mpana zaidi ya kuutazama kama mfumo unaowapa wanaume mamlaka dhidi ya wanawake. Nadharia hii iliruhusu kuchanganua pia gharama zinazoweza kuwapata wanaume wanapojaribu kufikia au kudumisha viwango vya uanaume vinavyotambuliwa na jamii. Hivyo, katika uchanganuzi wa *Nguu za Jadi* na *Penzi la Damu*, vipengele vya mamlaka na udhibiti, kujitegemea na utoaji wa huduma, uthubutu na ukakamavu, ukandamizaji wa kihisia, ushindani na mafanikio, pamoja na utawala katika mahusiano ya kijinsia vitatumika kama vigezo vya kubainisha namna matarajio ya ubabedume yanavyohusishwa na kudhoofika kwa afya ya kimwili, matatizo ya afya ya akili, hasara za kifedha, kuvurugika kwa mahusiano, upweke, kifungo na kuhatarisha maisha ya wahusika wa kiume.

## MBINU ZA UTAFITI

Makala hii ilitumia mkabala wa kimaelezo wenye mwelekeo wa kiufafanuzi na uchanganuzi wa yaliyomo ya kifasihi. Utafiti ulilenga kuchanganua namna matarajio ya ubabedume yanavyojengwa katika matini na jinsi yanavyohusishwa na dhiki zinazowakumba wahusika wa kiume. Uchanganuzi wa yaliyomo ulifaa kwa sababu uliwezesha mtafiti kutambua, kuainisha na kufasiri mifumo ya maana inayojitokeza katika matini za kifasihi (Kothari, 2004).

Data ya utafiti ilitokana na riwaya mbili za Kiswahili zilizoandikwa na waandishi wanawake, ambazo ni *Nguu za Jadi* (2019) ya Clara Momanyi na *Penzi la Damu* (2017) ya Anna Manyanza. Riwaya hizi ziliteuliwa kimakusudi kwa kuzingatia uhusiano wake na suala la utafiti. Uteuzi wa kimakusudi uliwezesha kuchagua matini ambazo wahusika wa kiume wanakabiliwa na matarajio, kanuni na shinikizo zinazohusishwa na uanaume na ubabedume. Creswell na Creswell (2018) wanaeleza kuwa usampulishaji wa kimakusudi huwezesha mtafiti kuchagua vyanzo vyenye taarifa zinazohusiana moja kwa moja na jambo linalochunguzwa.

Ukusanyaji wa data ulifanywa kwa hatua kadhaa. Kwanza, riwaya zote mbili zilisomwa kwa kina ili kupata uelewa wa jumla wa visa, wahusika, mahusiano na migogoro inayojitokeza katika matini. Pili, wakati wa usomaji wa pili, vifungu vyenye taarifa kuhusu matarajio ya kijamii ya uanaume vilitambuliwa. Vifungu hivyo vilihusisha maelezo ya msimulizi, mazungumzo ya wahusika, vitendo, mawazo, migogoro na matukio yaliyodhihirisha matarajio kuhusu mwanaume kuwa mwenye mamlaka, mtoa huduma, jasiri, mwenye nguvu, mshindani, anayejitegemea na asiyeonyesha udhaifu. Tatu, vifungu vilivyotambuliwa vilirekodiwa pamoja na

taarifa za mahali vilipotokea katika riwaya, mhusika anayehusika, mazingira ya tukio na aina ya matarajio ya kijinsia yaliyojitokeza.

Nne, data hizo ziliainishwa katika makundi mawili yanayohusiana: kwanza, vipengele vya ubabedume vilivyojitokeza katika matini, ambavyo ni mamlaka na udhibiti, kujitegemea na jukumu la mtoa huduma, uthubutu na ukakamavu, ukandamizaji wa kihisia, ushindani na mafanikio, pamoja na utawala katika mahusiano ya kijinsia; pili, aina za dhiki zilizohusishwa na matarajio hayo, ambazo ni kudhoofika kwa afya ya kimwili, matatizo ya afya ya akili, hasara au matatizo ya kifedha, kuvurugika kwa mahusiano, kupoteza heshima na hadhi na kuhatarisha maisha. Uainishaji huu uliwezesha kutenganisha matarajio ya ubabedume na matokeo yake huku ukifuatilia uhusiano kati ya vipengele hivyo.

Tano, data zililinganishwa ndani ya kila riwaya na kati ya riwaya hizo mbili ili kubaini mifumo inayojirudia, tofauti na mahusiano kati ya aina za matarajio ya ubabedume na dhiki zinazowakumba wahusika wa kiume. Kwa mfano, pale ambapo wahusika walitarajiwa kuwa watoa huduma, mtafiti alichunguza iwapo matarajio hayo yaliambatana na matatizo ya kiuchumi, kupoteza hadhi au migogoro ya kifamilia. Vivyo hivyo, pale ambapo wahusika walitarajiwa kuwa wakakamavu na wasiokuwa na udhaifu, data zilichunguzwa ili kubaini kama matarajio hayo yaliambatana na ukandamizaji wa hisia, tabia hatarishi, migogoro au matatizo ya afya ya akili.

Uaminifu na uthabiti wa uchanganuzi vilihakikishwa kwa kufuata utaratibu unaofanana katika uchambuzi wa data kutoka katika riwaya zote mbili. Mtafiti alirejea vifungu vilivyoteuliwa mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa tafsiri ilizingatia muktadha wa matukio, wahusika na mahusiano yao katika matini. Aidha, data ziliainishwa kwa kutumia vigezo vilevile katika riwaya zote mbili, na ulinganishaji wa data ulifanywa ndani ya kila riwaya na kati ya riwaya hizo mbili ili kuthibitisha mifumo iliyojitokeza. Ufafanuzi wa data uliongozwa na dhana za Nadharia ya Ubabedume ya Connell (1995), hasa uanaume tawala na mahusiano ya nguvu, ili kuhakikisha kuwa uchanganuzi una mwelekeo thabiti wa kinadharia. Vilevile, mada na mahusiano yaliyobainishwa yalitegemezwa na ushahidi wa moja kwa moja kutoka katika matini badala ya kutegemea tukio au mfano mmoja. Hatua hizi zilisaidia kupunguza uwezekano wa tafsiri za kibinafsi na kuimarisha uaminifu na uthabiti wa matokeo ya uchanganuzi.

Hatimaye, vifungu vilivyoteuliwa vilifasiriwa kwa kutumia Nadharia ya Ubabedume ya Connell (1995), hasa dhana ya uanaume tawala na mahusiano ya nguvu. Uchanganuzi haukuishia kubainisha kwamba tukio fulani lilitokea, bali ulitafuta kueleza namna tukio hilo lilivyohusiana na matarajio ya kijamii kuhusu uanaume na jinsi matarajio hayo yalivyozalisha au kuchangia dhiki kwa mhusika. Matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya uchanganuzi wa mada, yakitegemezwa na ushahidi wa matini kutoka katika riwaya teule na kuhusishwa na tafiti zilizopo kuhusu ubabedume, uanaume na athari za majukumu ya kijinsia.

## MATOKEO NA MJADALA

Uchambuzi wa riwaya *Nguu za Jadi* na *Penzi la Damu* umebainisha kuwa ubabedume hujengwa kupitia matarajio ya kijamii yanayowataka wanaume kuwa wenye mamlaka, jasiri, wakakamavu, wanaojitegemea, watoa huduma na wasioonyesha udhaifu wa kihisia. Matarajio hayo yanaweza kuwapa wanaume hadhi na mamlaka katika mazingira fulani, lakini pia huwasababishia dhiki zinapokuwa vigumu kuyatimiza au zinapowalazimisha kufanya maamuzi yenye madhara kwao wenyewe na kwa wengine. Dhiki zilizobainika katika riwaya hizi zinahusu kudhoofika kwa afya ya kimwili na kiakili, matatizo ya kiuchumi, kuvurugika kwa mahusiano, kupoteza heshima na hadhi, pamoja na kuhatarisha maisha. Matokeo haya yanaonyesha pia kuwa athari za ubabedume hazijitokezi kwa namna moja katika riwaya zote mbili; zinategemea mazingira, nafasi ya mhusika na aina ya matarajio ya kijinsia anayokabiliana nayo. Kwa msingi huo, mjadala unaofuata unalinganisha namna riwaya hizi zinavyowasilisha dhiki za wanaume, ukihusisha ushahidi wa matini na misingi ya Nadharia ya Ubabedume pamoja na tafiti zilizotangulia ili kubainisha maeneo ya mwafaka, tofauti na mchango wa utafiti huu.

### Ubabedume na Kudhoofika kwa Afya ya Kimwili

Uchambuzi wa *Nguu za Jadi* na *Penzi la Damu* umebainisha kuwa matarajio ya ubabedume yanaweza kuhusishwa na kudhoofika kwa afya ya kimwili kwa njia tofauti. Katika riwaya hizi, uanaume umejengwa kupitia matarajio ya kujitegemea, uhuru wa kufanya maamuzi, ukakamavu na kutokubali kuonekana dhaifu. Hata hivyo, matarajio hayo yanapotekelezwa bila kuzingatia ustawi

wa mwanaume, huweza kumweka katika mazingira yanayohatarisha afya yake.

Katika *Nguu za Jadi*, hali hii inadhihirika kupitia mhusika Mrima, ambaye baada ya kuitelekeza familia yake anazama katika ulevi na maisha ya anasa akikaidi ushauri na maaso ya mkewe, Mangwasha. Kwa mtazamo wa kijamii, mwenendo huu unahusishwa na dhana kwamba mwanaume ana mamlaka ya kufanya maamuzi yake binafsi bila kuhojiwa au kudhibitiwa na wengine. Mwenendo wake unaonyesha namna dhana ya uhuru wa mwanaume inaweza kugeuka kuwa kujitawala bila uwajibikaji kwa wengine au kwa afya yake mwenyewe. Mbungulu anapomwona baada ya muda mrefu anasema:

Aah, Mrima amesalia gofu! Kakonda hata ukimpulizia pumzi ataanguka. Kasalia kamba ya mbuzi mwenzangu. Mchafu kama fungo. Amelewa chakari, hatazamiki. (uk. 97)

Ushahidi huu hauonyeshi tu kuzorota kwa mwili wa Mrima, bali pia kinyume kati ya taswira ya nguvu inayohusishwa na uanaume na hali halisi ya mwanaume anayetekeleza baadhi ya matarajio hayo. Uhuru na kujitegemea, ambavyo vinaweza kutazamwa kama sifa za mwanaume mwenye uwezo wa kujiongoza, vinageuka kuwa chanzo cha kujitelekeza na matumizi mabaya ya pombe. Kwa mtazamo wa Connell (1995), ubabedume hujengwa kupitia kanuni zinazoweka viwango vya uanaume vinavyotakiwa kutambuliwa na jamii. Katika kisa cha Mrima, tatizo si uhuru wenyewe, bali namna unavyounganishwa na maisha ya starehe na kutokuwajibika, hali inayosababisha madhara ya moja kwa moja kwa afya yake.

Kwa upande wa *Penzi la Damu*, kudhoofika kwa afya ya kimwili kunajitokeza kupitia Huseni kwa namna tofauti. Baada ya kufiwa na mkewe Odette pamoja na mwanawe wa kwanza wakati wa kujifungua, Huseni anakumbwa na majonzi makubwa yanayotikisa maisha yake. Hata hivyo, badala ya kukabiliana na majonzi hayo kwa njia ya kawaida kama kushirikisha wengine hisia zake au kutafuta faraja kutoka kwa familia na jamii, anachagua kitendo cha hatari cha kujirusha kutoka juu ya mnazi. Kitendo hiki kinaonyesha jinsi matarajio ya mwanaume kuwa mkakamavu, jasiri, mwenye uthubutu na asiyeonyesha udhaifu wa kihisia yanavyoweza kumzuia kukabiliana na maumivu kwa njia salama. Matokeo ya kitendo hicho ni madhara makubwa ya kimwili. Huseni anapata majeraha yanayosababisha ulemavu wa kudumu ambapo mkono wake wa kushoto unajikunja kifuani na mguu wake wa kushoto unabaki ukibururuka.

Kwa hiyo, ingawa Mrima na Huseni wanakabiliwa na mazingira tofauti, riwaya zote mbili zinaonyesha mwili wa mwanaume kama eneo linalobeba gharama za matarajio ya ubabedume. Mrima anadhurika kutokana na matumizi mabaya ya pombe na maisha ya kujitelekeza, ilhali Huseni anapata ulemavu kutokana na hatua ya kujidhuru inayohusishwa na kushindwa kukabiliana na majonzi. Tofauti hii ni muhimu kwa sababu inaonyesha kuwa dhiki ya kimwili inayohusishwa na ubabedume haitokani na tabia moja pekee; inaweza kuzalishwa na namna tofauti za kutekeleza au kushindwa kutekeleza matarajio ya uanaume.

Matokeo haya yanaafikiana na Courtenay (2000), ambaye anaonyesha kuwa baadhi ya kanuni za uanaume wa jadi zinaweza kuwahusisha wanaume na mienendo inayohatarisha afya. Vilevile, yanaendana na Connell (1995) kwamba uanaume hujengwa kijamii kupitia matarajio na mahusiano ya nguvu. Hata hivyo, uchanganuzi wa riwaya hizi unaongeza katika mjadala huo kwa kuonyesha kifasihi kwamba gharama za ubabedume zinaweza kujidhihirisha kupitia njia zinazokinzana: mwanaume anaweza kudhuriwa na uhuru usio na uwajibikaji, kama ilivyo kwa Mrima, au na ukakamavu unaomzuia kukiri maumivu na kutafuta msaada, kama ilivyo kwa Huseni. Kwa mtazamo huu, waandishi wanawake wanaonyesha kwamba sifa zinazotambuliwa kijamii kama alama za nguvu za kiume zinaweza, katika mazingira fulani, kugeuka kuwa vyanzo vya udhaifu, majeraha na kuzorota kwa afya ya mwanaume.

**Ubabedume na Matatizo ya Afya ya Akili**

Riwaya teule mbili zimebainisha kuwa ubabedume unaweza kuhusishwa na matatizo ya afya ya akili pale ambapo utambulisho wa mwanaume unajengwa kwa kutegemea mamlaka, hadhi, ukakamavu na uwezo wa kuvumilia matatizo bila kuonyesha udhaifu. Katika riwaya hizi, dhiki ya kisaikolojia inajitokeza kwa njia tofauti kulingana na mazingira ya wahusika. Akiwa mwanasiasa mwenye ushawishi mkubwa na baba wa familia, Sagilu katika *Nguu za Jadi* amejenga utambulisho wake wa kijinsia juu ya misingi ya mamlaka, udhibiti na uwezo wa kutawala wengine. Kwa muda mrefu, anatumia nafasi yake ya kijamii na kisiasa kujihakikishia heshima na utiifu kutoka kwa watu wanaomzunguka. Hata hivyo, msingi huo wa uanaume

unaanza kuyumba baada ya siri zake kufichuliwa na uhusiano wake na familia kuvurugika.

Tatizo linaanza pale ambapo Ngoswe anafichua ukweli kuhusu tabia zake za kimapenzi, jambo linalopelekea kuporomoka kwa hadhi yake ya kijamii. Hali inakuwa mbaya zaidi mwanawe Mashauri anapomkana na kujiunga na wapinzani wake wa kisiasa. Matukio haya yanamwondolea Sagilu mambo ambayo alikuwa ameyategemea kujitambulisha kama mwanaume mwenye mafanikio na mamlaka. Badala ya kuonekana kama kiongozi mwenye heshima, anaanza kutengwa na kulaumiwa na watu waliokuwa karibu naye.

Kadhia hii inaonyesha kuwa kwa Sagilu, mamlaka na udhibiti si nyenzo za uongozi pekee, bali ni sehemu ya utambulisho wake kama mwanaume. Kwa hiyo, anapopoteza uwezo wa kudhibiti watu na mazingira yaliyokuwa yanamthibitishia hadhi, anakumbwa na mgogoro wa kisaikolojia na kuishia kuwa mwendawazimu. Hali hii inaeleweka kupitia Connell (1995), anayeeleza kuwa ubabedume hujenga aina ya uanaume inayohusishwa na mamlaka na hadhi ya juu. Hivyo, pale thamani ya mwanaume inapofungamanishwa kwa kiasi kikubwa na uwezo wake wa kutawala, kupoteza mamlaka kunaweza kuwa tishio kwa utambulisho wake na kuzalisha dhiki ya kisaikolojia. Katika kisa cha Sagilu, mwandishi anaonyesha kwa namna hii gharama ya kisaikolojia ya kujenga uanaume juu ya mamlaka na udhibiti.

Katika *Penzi la Damu*, tatizo la afya ya akili linajitokeza kwa Kayeba Mirambo, ambaye anarudi kutoka Vita Vikuu vya Pili vya Dunia akiwa na athari za kisaikolojia za uzoefu wa vita. Kama mwanaume anayetarajiwa kuwa mlinzi na mtetezi wa taifa, anashiriki katika vita bila matarajio ya wazi kwamba jukumu hilo linaweza kumwacha na majeraha ya muda mrefu ya kisaikolojia. Baada ya kurejea, anaanza kuonyesha dalili za msongo wa mawazo baada ya ntwe (*Post-Traumatic Stress Disorder*). Anasumbuliwa na ndoto za vita, mauaji na mateso, anapiga kelele usingizini na wakati mwingine anatoka nje bila kujitambua:

...alikuwa akiandamwa na ndoto za kutisha usiku. Aliota ndoto za vita, ndoto za mauaji…mateso…Kila mara alipiga kelele na kuamka huku yu bado usingizini. Alitoka nje bila kujijua. Alikuwa kama mwehu... (uk. 33).

Kulingana na ushahidi huu, inaonyeshwa kuwa jukumu la mwanaume kama mlinzi na shujaa lina gharama inayoweza kuendelea hata baada ya mazingira ya hatari kumalizika. Kinachodhihirika katika simulizi hili ni kwamba matarajio ya ubabedume yanamzuia Mirambo kueleza wazi maumivu yake ya kihisia. Badala ya kutafuta msaada au kuzungumzia yale aliyopitia vitani, analazimika kubeba mateso yake kimya kimya kwa sababu jamii inamtarajia kuendelea kuwa imara na jasiri. Hali hii inaongeza mzigo wa kisaikolojia anaoubeba na kufanya mchakato wa kupona kuwa mgumu zaidi. Mirambo anabeba majeraha yasiyoonekana ya uzoefu wa vita, huku matarajio ya ukakamavu na ujasiri yakimwekea mazingira ya kuvumilia mateso hayo badala ya kuyatambua na kutafuta msaada. Kwa mtazamo wa ubabedume, ukakamavu unaotarajiwa kutoka kwa mwanaume unaweza hivyo kuwa kikwazo katika kutambua na kushughulikia maumivu ya kihisia na kisaikolojia.

Kulinganisha Sagilu na Mirambo kunaonyesha aina mbili tofauti za chanzo cha dhiki ya afya ya akili ndani ya mfumo wa ubabedume. Sagilu anateseka kutokana na kupoteza mamlaka, heshima na udhibiti alioujenga kama msingi wa utambulisho wake, wakati Mirambo anabeba athari za kisaikolojia za kutekeleza jukumu la kijamii la kuwa mlinzi na shujaa na kuogopa kushiriki na wengine, dhiki zilizotokana na vita. Tofauti hii inaonyesha kuwa dhiki ya mwanaume haitokani na kushindwa kwa aina moja ya matarajio; inaweza pia kuzalishwa na gharama za kuyatimiza matarajio hayo. Kwa maana hiyo, mwanaume anaweza kuathirika anaposhindwa kuwa mwenye mamlaka, lakini pia anaweza kuathirika kwa sababu ya kulazimika kuwa jasiri na mvumilivu katika mazingira hatarishi.

Hoja hii inalingana na Kimmel (2008), anayebainisha kuwa matarajio ya jamii kuhusu mafanikio, nguvu na uwezo wa mwanaume yanaweza kumweka katika shinikizo la kudumu, pamoja na O'Neil (2008), anayehusisha matarajio magumu ya majukumu ya kijinsia na migogoro ya kisaikolojia. Hata hivyo, uchanganuzi wa riwaya hizi unaongeza katika mjadala huo kwa kuonyesha kwamba dhiki ya afya ya akili inayohusishwa na ubabedume inaweza kuzalishwa na pande mbili za uanaume: kulinda hadhi na mamlaka, na kutekeleza wajibu wa ulinzi kwa gharama ya hisia na ustawi binafsi. Kwa hiyo, *Nguu za Jadi* na *Penzi la Damu* zinafichua kuwa ubabedume haujengi tu taswira ya mwanaume mwenye nguvu, bali pia unaweza

kuzalisha sononeko, mfadhaiko, hofu na kuporomoka kwa utulivu wa akili pale matarajio hayo yanaposhindikana au yanapotekelezwa kwa gharama kubwa kwa mwanaume mwenyewe.

**Ubabedume na Dhiki za Kiuchumi**

Uchanganuzi wa *Nguu za Jadi* na *Penzi la Damu* umebainisha kuwa ubabedume unaweza kuzalisha dhiki za kiuchumi pale ambapo thamani ya mwanaume inahusishwa na uwezo wa kifedha, mamlaka ya kufanya maamuzi na kutekeleza wajibu wa kuwa mtoa huduma wa familia. Katika riwaya hizi, matarajio hayo yanawaweka wahusika wa kiume katika mazingira ambayo maamuzi ya kuthibitisha uanaume wao huishia kuhatarisha mali, kipato na ustawi wa familia.

*Nguu za Jadi* inaonyesha Sagilu akijenga sehemu ya utambulisho wake wa kiume juu ya utajiri na uwezo wa kutumia mali kuthibitisha hadhi na mvuto wake. Uhusiano wake na Sihaba unaonyesha wazi hali hii:

Pesa kwake zilikuwa kigezo cha penzi. Sagilu alimpa (Sihaba) chochote alichotaka. Alimjengea jumba kubwa, akamnunulia gari la kifahari… (uk. 16).

Ushahidi huu unaonyesha kwamba mali si rasilimali ya kiuchumi pekee kwa Sagilu, bali pia ni nyenzo ya kuthibitisha uwezo na hadhi yake kama mwanaume. Anapotumia fedha kujenga nyumba, kununua gari na kugharamia mahitaji ya wanawake anaohusiana nao (Sihaba na Cheiya), anatimiza matarajio ya uanaume yanayomweka mwanaume katika nafasi ya mwenye uwezo wa kutoa na kumiliki. Hata hivyo, matumizi hayo yanaweka utajiri wake katika mahusiano ambayo msingi wake mkubwa ni uwezo wa kifedha. Baada ya kupoteza ushawishi wake wa kisiasa na kuanguka kiuchumi, Sagilu anajikuta amepoteza sehemu kubwa ya mali yake. Wanawake ambao aliwategemea kama sehemu ya maisha yake wanamwacha, huku yeye akibaki katika hali ya umaskini na kukata tamaa. Mwandishi anaonyesha kuwa uhusiano uliokuwa umejengwa juu ya uwezo wa kifedha haukuwa na msingi imara wa kijamii wala wa kihisia. Kwa hivyo, kile kilichotumika kujenga hadhi yake ya kiume kinageuka kuwa chanzo cha hasara na kuporomoka kwa maisha yake.

Katika *Penzi la Damu*, dhiki ya kiuchumi inajitokeza kupitia Baba Msimbazi, ambaye anatumia mamlaka yake ya kibabedume kufanya maamuzi yanayoathiri mali na ustawi wa familia. Anapuuza ushauri wa mkewe kuhusu hatari ya kuwaamini waganga wanaomwahidi utajiri na mafanikio, akiamini kuwa yeye ndiye mwenye kauli ya mwisho katika familia. Hatimaye, anatumia mali ya familia katika shughuli zisizo na manufaa na hatimaye kulazimika kuuza mashamba pamoja na nyumba ya familia. Matokeo yake ni kuporomoka kwa hali ya kiuchumi ya familia na kupungua kwa uwezo wake wa kutekeleza wajibu wa ukimu.

Hali hii inaonekana pia katika namna Baba Msimbazi anavyohusisha uanaume na uzazi mkubwa. Ana watoto saba, wavulana sita na msichana mmoja, na idadi hiyo anaiona kama ishara ya nguvu na uwezo wake wa kiume. Hata hivyo, baada ya kuhamia mjini, anashindwa kukidhi mahitaji ya familia hiyo kubwa, hali inayosababisha msongamano kwenye chumba kimoja alichomudu na upungufu wa mahitaji muhimu. Hivyo, riwaya inaonyesha kinaya cha matarajio ya uzazi: kile kinachoweza kumpa mwanaume hadhi kama mwenye "nguvu za kiume" wakati mmoja kinaweza kumletea mzigo mkubwa wa kiuchumi anaposhindwa kukidhi mahitaji ya familia yake.

Kwa kulinganisha riwaya hizi mbili, Sagilu na Baba Msimbazi wanadhurika kiuchumi kupitia njia tofauti lakini zinazotokana na msingi mmoja wa ubabedume—thamani ya mwanaume kupimwa kwa uwezo wake wa kumiliki, kutoa na kutawala. Sagilu anatumia utajiri kuthibitisha hadhi yake katika mahusiano ya kimapenzi, ilhali Baba Msimbazi anatumia mamlaka yake kufanya maamuzi ya kifamilia na pia anahusisha uanaume na uzazi mkubwa. Tofauti hii inaonyesha kuwa dhiki ya kiuchumi inayohusishwa na ubabedume haiishii katika kushindwa kupata kipato; inaweza pia kusababishwa na matumizi ya mali ili kuthibitisha hadhi, maamuzi yasiyoshauriwa yanayofanywa kwa misingi ya mamlaka ya kiume, au ukubwa wa majukumu ya kifamilia unaotokana na matarajio ya kijinsia.

Matokeo haya yanawafiki maoni ya Silberschmidt (2001), ambaye anaonyesha kuwa uwezo wa mwanaume kutimiza jukumu la mtafutaji na mtoa huduma una uhusiano mkubwa na hadhi na utambulisho wake katika mazingira ya Kiafrika. Vilevile, yanaendana na Connell (1995) kwamba ubabedume huhusisha uanaume na mamlaka, rasilimali na nafasi ya juu katika mahusiano ya kijamii. Hata hivyo, riwaya hizi zinaongeza katika mjadala huo kwa kuonyesha kinaya cha kiuchumi cha ubabedume: rasilimali zinazotumiwa kujenga mamlaka na hadhi ya mwanaume zinaweza hatimaye kuwa chanzo cha kupoteza mali, umaskini na kushindwa kutekeleza

majukumu ya kifamilia. Kwa hiyo, *Nguu za Jadi* na *Penzi la Damu* zinaonyesha kwamba matarajio ya mwanaume kuwa mwenye mali, mtoa huduma na mwenye mamlaka yanaweza kumpa hadhi, lakini yakitekelezwa bila uwiano yanaweza pia kumweka katika mazingira ya dhiki ya kiuchumi na kuathiri ustawi wa familia yake.

**Ubabedume na Kuvurugika kwa Mahusiano**

Kuvurugika kwa mahusiano ni mojawapo ya gharama za ubabedume zinazojitokeza katika riwaya *Nguu za Jadi* na *Penzi la Damu*. Uchanganuzi wa matini unaonyesha kuwa matarajio ya mwanaume kuwa mwenye mamlaka, udhibiti na haki ya kufanya maamuzi bila kupingwa yanaweza kudhoofisha mahusiano ya kifamilia na kijamii. Katika *Nguu za Jadi*, hali hii inadhihirika kupitia Sagilu, ambaye anatumia nafasi yake kama baba na mwanasiasa mwenye mamlaka kujihusisha kimapenzi na Cheiya, mchumba wa mwanawe Mashauri. Kitendo hiki kinaonyesha namna mamlaka ya kibabedume yanavyoweza kumjengea mwanaume hisia ya kwamba nafasi yake inampa uhuru wa kutanguliza matakwa yake binafsi bila kuzingatia mipaka ya mahusiano.

Madhara ya matumizi hayo ya mamlaka yanaonekana pale Mashauri anapogundua uhusiano huo na kupoteza imani na heshima kwa baba yake. Uhusiano wao unavurugika kiasi cha Mashauri kujitenga na Sagilu na hata kumpinga katika uwanja wa kisiasa. Hivyo, kile Sagilu anachokitumia kama ishara ya mamlaka na uhuru wa kiume kinageuka kuwa chanzo cha kupoteza uhusiano muhimu wa kifamilia. Hali hiyo inajitokeza pia katika uhusiano wake na Ngoswe, rafikiye Mashauri. Inafahamika baadaye kuwa Ngoswe ni mwanawe Sagilu. Alizaliwa kutokana na uhusiano wa kisiri wa Sagilu na mke wa Mtemi Lesulia. Ngoswe anapofahamu ukweli kuhusu nasaba yake, naye anapoteza heshima kwake. Hatimaye Sagilu anajikuta ametengwa na watoto wake na kupoteza nafasi yake kama nguzo ya familia. Hali hii inamwathiri pia kisaikolojia kwa sababu anakosa mahusiano ya karibu yaliyokuwa sehemu muhimu ya maisha yake. Kwa mtazamo wa ubabedume, hali hii inaonyesha kinzani muhimu: juhudi za kudumisha mamlaka ya kiume zinaweza kumfanya mwanaume apoteze mahusiano ambayo mamlaka hayo yanakusudiwa kuyatawala na kuyadumisha.

Katika *Penzi la Damu*, kuvurugika kwa mahusiano kunajengwa zaidi kupitia ukali na udhibiti wa Baba Msimbazi ndani ya familia. Anaamini kuwa mwanaume ndiye mwenye mamlaka ya mwisho katika nyumba na kwamba mke na watoto wanapaswa kutii maamuzi yake bila kuyahoji, hali inayomfanya kumdhalilisha na kumpiga mkewe mara kwa mara:

> Mama Msimbazi kila kulipokucha alichapwa makofi na mumewe…Baba Msimbazi alikuwa na mkono mwepesi…kipigo cha kila siku kilimchakaza mkewe… (uk. 7).

Ushahidi huu unaonyesha kuwa mamlaka ya kibabedume hayajengwi kwa maamuzi pekee, bali pia kupitia matumizi ya nguvu za kimwili kama njia ya kudhibiti familia. Matokeo yake ni kuibuka kwa hofu, chuki na kujitenga badala ya ukaribu na mshikamano. Ukali huu ulifanya mkewe na wanawe kujikunyata kama vipanya yatima aliporejea nyumbani. Mkewe aliona kuwa mumewe hamjali. Vitendo hivi vinazalisha mazingira ya hofu na chuki badala ya upendo na ushirikiano wa kifamilia. Watoto wake wanaanza kumuogopa badala ya kumheshimu, huku mkewe akijitenga na kushindwa kushiriki kikamilifu katika masuala ya familia. Mke na watoto wanamwogopa Baba Msimbazi badala ya kumwona kama chanzo cha usalama na ushirikiano. Aidha, anapojimilikisha mamlaka yote ya kufanya maamuzi ya kifedha na kupuuza maoni ya mkewe, anazidisha migogoro ya kifamilia na kudhoofisha zaidi mahusiano yake na wanafamilia.

Ingawa Sagilu na Baba Msimbazi wanatofautiana katika namna wanavyotumia mamlaka, matendo yao yanaonyesha muundo unaofanana wa ubabedume. Sagilu anatumia mamlaka na hadhi yake kutanguliza tamaa binafsi, ilhali Baba Msimbazi anatumia ukali, nguvu na udhibiti kuhakikisha familia inatii maamuzi yake. Katika visa vyote viwili, matarajio ya mwanaume kuwa mtawala wa familia hayazalishi mshikamano unaotarajiwa, bali yanamnyang'anya mwanaume mahusiano ya karibu. Sagilu anapoteza uaminifu wa wanawe, huku Baba Msimbazi akipoteza ukaribu, upendo na heshima ya mke na watoto wake. Tofauti hiyo inaonyesha kuwa gharama ya ubabedume inaweza kujitokeza kupitia njia mbalimbali, lakini matokeo yake yanaweza kuwa sawa: kutengwa kwa mwanaume na watu ambao ni muhimu kwa ustawi wake wa kijamii na kihisia.

Matokeo haya yanakubaliana na Connell (1995), anayehusisha ubabedume na mahusiano ya nguvu ambapo aina fulani ya uanaume hupewa uwezo wa kutawala na kudhibiti wengine. Hata hivyo, mifano ya

riwaya hizi inaongeza kipengele ambacho hakijitokezi wazi katika mtazamo unaouona ubabedume hasa kama mfumo wa mamlaka: mamlaka ya mwanaume yanaweza kumrudia mwenyewe kama chanzo cha dhiki. Sagilu na Baba Msimbazi wanapotumia mamlaka ya kibabedume kudhibiti wengine, matokeo yake ni kupoteza uaminifu, ukaribu na mshikamano wa kifamilia. Kwa hiyo, riwaya hizi zinaonyesha kuwa nguvu inayotumika kujenga na kulinda hadhi ya mwanaume inaweza wakati huo huo kuharibu mahusiano yanayompa mwanaume usalama wa kijamii na kihisia.

Kwa mtazamo huo, waandishi wa riwaya hizi wanafichua sura nyingine ya gharama za ubabedume: mwanaume anaweza kuwa mtawala wa familia lakini akawa mpweke ndani ya familia hiyo hiyo. Hivyo, kuvurugika kwa mahusiano si athari ya pembeni ya ubabedume, bali ni mojawapo ya gharama zinazotokana moja kwa moja na matarajio ya mamlaka, udhibiti na ukuu wa kiume. Utafiti huu, kwa hiyo, unaongeza katika mjadala wa uanaume katika fasihi ya Kiswahili kwa kuonyesha kwamba uchanganuzi wa ubabedume unapaswa kuzingatia si tu nani anayepata mamlaka, bali pia gharama ambazo mwanaume mwenyewe hulipa anapotumia au kulinda mamlaka hayo.

**Ubabedume na Kupoteza Heshima na Hadhi ya Mwanaume**

Kupoteza heshima na hadhi ni mojawapo ya gharama za ubabedume zinazojitokeza katika *Nguu za Jadi* na *Penzi la Damu*. Uchanganuzi wa matini unaonyesha kuwa wahusika wa kiume hujenga hadhi zao kwa kutegemea mamlaka, uwezo wa kiuchumi, udhibiti na ubabe dhidi ya wengine. Hata hivyo, misingi hiyo ya uanaume huwa dhaifu kwa sababu hadhi inayotegemea uwezo wa kumiliki, kutawala au kudhibiti wengine inaweza kuporomoka mara tu mamlaka hayo yanapotikiswa.

Katika *Nguu za Jadi*, Sagilu anajenga utambulisho wake wa kiume kupitia utajiri, mamlaka ya kisiasa na uwezo wa kuwatawala wanawake. Mali anazomiliki na ushawishi alionao vinakuwa nyenzo za kuthibitisha mafanikio na hadhi yake mbele ya jamii. Hata hivyo, uhusiano wake wa kimapenzi na wanawake mbalimbali, hususan Cheiya ambaye ni mchumba wa mwanawe Mashauri, unageuka kuwa chanzo cha anguko lake. Mahusiano yake ya kimapenzi na wanawake mbalimbali, hususan Cheiya ambaye ni mchumba wa mwanawe Mashauri, yanamwondolea heshima aliyokuwa ameijenga kwa miaka mingi. Anapofumaniwa katika uhusiano huo, jamii inaanza kumwona kama mtu asiyezingatia maadili ya kifamilia na kijamii. Kushindwa kwake katika uchaguzi wa uwakilishi wa eneo la Matango kunakamilisha kuporomoka kwa hadhi yake ya kijamii na kisiasa.

Kwa upande mwingine, *Penzi la Damu* linawasilisha kupotea kwa hadhi kupitia mhusika Kasimu, ambaye anajenga taswira yake ya uanaume kwa kuwadharau na kuwanyanyasa wanafunzi wasichana shuleni. Kasimu anaamini kuwa wanaume ni viumbe wenye nguvu na mamlaka zaidi kuliko wanawake. Kwa sababu hiyo, anatumia lugha ya kejeli, matusi na dharau dhidi ya wasichana ili kudhihirisha ubabe wake mbele ya wanafunzi wenzake.

Kwa muda fulani, tabia hiyo inamfanya aonekane mwenye nguvu na ushawishi. Hata hivyo, hali inabadilika pale Malaika, mmoja wa wanafunzi wasichana anaowadharau, anapomkabili kwa kipigo hadharani. Katika tukio hilo, Kasimu anashindwa kudhibiti hali na kuishia kuaibishwa mbele ya wanafunzi wengine. Tukio hilo linamvunjia taswira aliyokuwa ameijenga ya mwanaume mwenye nguvu na mamlaka.

Kupitia tukio hili, mwandishi anaonyesha kuwa heshima inayojengwa kwa msingi wa kudhalilisha wengine huwa dhaifu na ya muda mfupi. Kasimu anapoteza hadhi yake kwa sababu msingi wa uanaume alioujenga ulitegemea unyanyasaji wa wanawake badala ya maadili ya kuheshimiana. Matokeo yake ni kudharauliwa na wanafunzi wenzake pamoja na kupoteza nafasi yake ya kijamii.

Tofauti kati ya Sagilu na Kasimu iko katika kiwango na mazingira ya matumizi ya mamlaka yao, lakini wote wanajenga hadhi kwa msingi wa aina ya uanaume unaohitaji kuthibitisha ubora, udhibiti na nguvu mbele ya wengine. Sagilu anategemea utajiri na mamlaka ya kisiasa, ilhali Kasimu anategemea ubabe na udhalilishaji wa wanawake. Katika visa vyote viwili, jitihada za kujenga na kudumisha taswira ya mwanaume mwenye nguvu huishia kuzaa matokeo kinyume: Sagilu anapoteza heshima, ushawishi na hadhi ya kifamilia na kisiasa, huku Kasimu akipoteza heshima mbele ya wenzake.

Matokeo haya yanaafikiana na Connell (1995) kwamba ubabedume huhusisha uanaume na mamlaka, hadhi na uwezo wa kudhibiti wengine, lakini pia huweka mwanaume katika hitaji la kuthibitisha nafasi hiyo mara

kwa mara. Kwa mtazamo huu, hadhi ya kibabedume si mali ya kudumu; hutegemea uwezo wa mwanaume kuendelea kuonyesha sifa zinazotambuliwa na jamii kuwa za kiume. Sagilu anapopoteza mamlaka ya kisiasa na kufichuliwa kwa mienendo yake isiyokubalika, msingi wa hadhi yake unatoweka. Vivyo hivyo, Kasimu anaposhindwa kudumisha ubabe wake mbele ya Malaika, taswira yake ya nguvu ya kiume inageuka kuwa chanzo cha fedheha.

Kwa hiyo, riwaya hizi zinaongeza katika mjadala wa ubabedume kwa kuonyesha kinzani kati ya kutafuta hadhi kupitia nguvu na matokeo ya kupoteza hadhi hiyo kwa sababu ya nguvu hizo hizo. Waandishi wanaonyesha kwamba heshima inayojengwa juu ya udhibiti wa wengine, utajiri au ukandamizaji inaweza kuwa ya muda mfupi na kumweka mwanaume katika hatari ya kupoteza utambulisho wake wa kijamii. Hivyo, kupoteza heshima na hadhi kunadhihirika si kama matokeo ya kushindwa kwa mtu binafsi pekee, bali kama gharama inayoweza kuzalishwa na matarajio ya ubabedume yenyewe.

**Ubabedume na Kuhatarisha Maisha**

Kuhatarisha maisha ni mojawapo ya gharama za ubabedume zinazojitokeza katika *Nguu za Jadi* na *Penzi la Damu*. Uchanganuzi wa matini unaonyesha kuwa matarajio yanayohusisha uanaume na ujasiri, uthubutu, ushupavu na ushindi wa kingono yanaweza kuwafanya wanaume kupuuza usalama wao wenyewe. Katika *Nguu za Jadi*, hali hii inadhihirika kupitia vijana wa taifa la Matuo wanaoshawishiwa na Mtemi Lesulia kushiriki katika vurugu za kisiasa katika maeneo ya Majengo na Matango ili kutetea maslahi ya viongozi wao. Mtemi Lesulia anawatumia vijana hao kama chombo cha kuimarisha ushawishi wake wa kisiasa kwa kuwapa fedha na kuwaelekeza kuzua vurugu. Kutokana na hali hiyo, vijana wanajikuta wakijiingiza katika mazingira yenye hatari kubwa ya kujeruhiwa au kupoteza maisha kwa ajili ya maslahi ambayo si yao.

Mwenendo huu unaonyesha namna matarajio ya ubabedume yanavyohusisha uanaume na ujasiri, ushupavu na utayari wa kukabiliana na hatari. Vijana hao wanasukumwa kuamini kwamba kuthubutu kushiriki katika mapambano ya kisiasa ni njia ya kuthibitisha uanaume wao na kuonyesha utii kwa mamlaka ya viongozi wa kiume. Hivyo, badala ya kutathmini athari za matendo yao, wanatanguliza taswira ya ukakamavu inayotukuzwa na jamii.

Hata hivyo, riwaya inaonyesha pia mtazamo tofauti kupitia mhusika Ngoswe ambaye anapinga matumizi ya vijana katika vurugu za kisiasa. Ngoswe anawaonya vijana wenzake dhidi ya kuhatarisha maisha yao kwa manufaa ya wanasiasa wanaowatumia kama nyenzo za kufanikisha malengo yao binafsi. Mtazamo huu unaonyesha kuwa si wanaume wote wanaokubali matarajio ya ubabedume yanayohusisha uanaume na matumizi ya nguvu au vurugu. Ngoswe anawaonya vijana wenzake dhidi ya kuhatarisha maisha yao kwa manufaa ya wanasiasa, akionyesha kwamba uanaume unaweza pia kujengwa kupitia uwezo wa kutafakari, kukataa vurugu na kulinda maisha.

Katika *Penzi la Damu*, hatari ya maisha inajitokeza kwa namna tofauti kupitia Bwana Shayo, anayehusishwa na mahusiano ya kingono yasiyo salama na Sheila, anayejulikana kwa jina la utani Cheupe Dawa. Sheila anasemekana kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanaume wengi, hususan madereva wa watalii, na kuna uvumi kwamba ameambukizwa virusi vya UKIMWI. Licha ya taarifa hizo, Shayo anapuuzia hatari hiyo na kuendelea kushiriki naye ngono isiyo salama:

Weupe wa Sheila na sketi zake za kubana zilizopasuliwa pembeni, na uzuri wake viliwavutia wanaume wengi. Ndio maana kulikuwa na uzushi kuwa alikuwa na virusi vya UKIMWI. Bwana Shayo hakujali tetesi zile… (uk. 101).

Kutojali kwake kunafichua namna hamu ya kuthibitisha uwezo wa kingono inaweza kushinda tahadhari inayohitajika katika kulinda afya. Katika muktadha wa ubabedume, uwezo wa kujihusisha na wanawake wengi na kuthubutu hatari pamoja na kutokuwa na hofu unaweza kutafsiriwa kama ishara ya nguvu za kiume. Kwa hiyo, Shayo anapopuuzia taarifa ya hatari, kitendo chake kinaweza kusomwa kama jitihada ya kudumisha taswira ya mwanaume jasiri na asiyeogopa. Hapa mwandishi anaonyesha kinzani ya ubabedume: kile kinachoweza kutambuliwa kama ujasiri wa kiume kinaweza wakati huohuo kuwa uzembe unaohatarisha afya na uhai.

Ingawa vijana wa Matuo na Shayo wanakabiliwa na mazingira tofauti, riwaya zote mbili zinaonyesha muundo unaofanana wa shinikizo la kuthibitisha uanaume kupitia hatari. Vijana wa *Nguu za Jadi* wanaingia katika vurugu kwa kushinikizwa na mamlaka za kisiasa, huku Shayo wa *Penzi la Damu* akipuuza hatari ya kiafya katika

harakati za kuridhisha tamaa ya kingono. Tofauti hii ni muhimu kwa sababu inaonyesha kuwa ubabedume hauzalishi hatari kwa njia moja tu: unaweza kutumika kisiasa kuwafanya wanaume wawe tayari kupigana, au kijamii na kingono kuwafanya wapuuze tahadhari zinazolinda maisha yao.

Matokeo haya yanaafikiana na Connell (1995), anayehusisha ubabedume na uanaume unaosisitiza uthubutu, ushindani na uwezo wa kudhihirisha nguvu. Hata hivyo, matini hizi zinaongeza jambo muhimu katika mjadala huo kwa kuonyesha gharama ya kimwili ya kuthibitisha uanaume kupitia hatari. Vijana wa Matuo wanakuwa wahanga wa mamlaka zinazowatumia kwa maslahi ya kisiasa, ilhali Shayo anaweka afya yake hatarini kutokana na msukumo wa kuthibitisha uwezo wake wa kingono. Kwa hivyo, hatari inayohusishwa na ubabedume haipaswi kueleweka kama sifa ya ujasiri pekee, bali pia kama utaratibu unaoweza kuwafanya wanaume kutanguliza uthibitisho wa uanaume kuliko usalama wao.

Kwa mtazamo huo, *Nguu za Jadi* na *Penzi la Damu* zinafichua kuwa baadhi ya matarajio yanayohusishwa na "uanaume halisi"—kama vile kutokuwa mwoga, kutumia nguvu, kuwa tayari kupambana na kuonyesha ushindi wa kingono—yanaweza kugeuka kuwa chanzo cha majeraha, magonjwa na vifo. Hivyo, mchango wa riwaya hizi katika mjadala wa ubabedume ni kuonyesha kwamba mwanaume anaweza kuwa mtekelezaji wa kanuni za ubabedume na wakati huohuo kuwa mhanga wa gharama zake.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho:** Makala hii imechunguza namna ubabedume unavyojitokeza kama chanzo cha dhiki kwa wahusika wa kiume katika riwaya za *Nguu za Jadi* na *Penzi la Damu* zilizoandikwa na waandishi wanawake. Kwa kutumia Nadharia ya Ubabedume ya Connell (1995), uchambuzi umeonyesha kuwa matarajio ya kijamii yanayohusisha uanaume na mamlaka, uthubutu, ukakamavu, uwezo wa kifedha, ushindi wa kingono na udhibiti wa wengine huwaweka wanaume katika shinikizo la kutimiza viwango vinavyoweza kuwa na gharama kubwa kwa maisha yao. Matokeo yamebainisha kuwa matarajio hayo huchangia kudhoofika kwa afya ya kimwili na kiakili, kuhasirika kifedha, kuvurugika kwa mahusiano ya kifamilia na kijamii, kupoteza heshima na hadhi pamoja na kuhatarisha maisha ya wanaume wenyewe.

Aidha, makala imeonyesha kuwa waandishi wanawake wa Kiswahili hawawachori wahusika wa kiume kama wanufaika wa mfumo wa ubabedume pekee, bali pia kama wahanga wa mfumo huo. Kupitia wahusika kama Mrima, Sagilu, Baba Msimbazi, Huseni, Kayeba Mirambo, Kasimu, Bwana Shayo na vijana wa Matuo, riwaya hizi zinafichua kuwa viwango vya ubabedume vinavyotukuzwa kijamii vinaweza kugeuka kuwa chanzo cha mateso, upweke, kuporomoka kwa ustawi na hata kuhatarisha uhai wa wanaume wanaojaribu kuvitimiza. Hivyo, makala hii inapanua mjadala wa fasihi ya Kiswahili kuhusu ubabedume kwa kuonyesha kuwa mfumo huo unaathiri jinsia zote, ingawa kwa namna tofauti, na kwamba ujenzi wa uanaume unaotegemea mamlaka, udhibiti na uthibitisho wa mara kwa mara unaweza kuwa mzigo badala ya manufaa kwa wanaume wenyewe.

**Mapendekezo:** Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huu, inapendekezwa kuwa tafiti za fasihi ya Kiswahili ziendelee kuchunguza ubabedume kwa kuzingatia kinzani kati ya mamlaka na gharama zake kwa wanaume. Badala ya kuuchukulia ubabedume kama mfumo unaowanufaisha wanaume pekee, tafiti zijazo zinapaswa kuangazia pia namna matarajio ya kijinsia yanavyoweza kuwafanya wanaume kuwa wahanga wa mfumo huo. Mtazamo huu utasaidia kupanua mjadala wa uanaume katika fasihi ya Kiswahili na kutoa uelewa mpana zaidi kuhusu namna ujenzi wa uanaume unavyoweza kuathiri ustawi wa mwanaume mwenyewe pamoja na mahusiano yake na wengine.

Aidha, inapendekezwa kuwa taasisi za elimu, wataalamu wa masuala ya jinsia na watunga sera waimarishe mijadala kuhusu miundo mbadala ya uanaume inayosisitiza uwajibikaji, ushirikiano, mawasiliano ya wazi, kuheshimiana na kuthamini afya ya kimwili na kiakili. Mijadala hiyo inapaswa kuhoji mitazamo inayomlazimisha mwanaume kujithibitisha kupitia mamlaka, matumizi ya nguvu, uwezo wa kifedha, ushindani, ushupavu usio na mipaka au ushindi wa kingono. Hatua hiyo inaweza kusaidia kujenga mitazamo ya uanaume inayomruhusu mwanaume kutafuta msaada, kueleza hisia zake, kufanya maamuzi kwa ushirikiano na kuzingatia ustawi wake bila kuona vitendo hivyo kama ishara ya udhaifu.

Vilevile, tafiti zijazo zinashauriwa kupanua wigo wa kifasihi na kimtazamo kwa kuchunguza ubabedume katika tanzu nyingine za fasihi ya Kiswahili, kama vile

tamthilia, ushairi na hadithi fupi, pamoja na kujumuisha kazi nyingi zaidi za waandishi wanawake na wanaume. Tafiti linganishi zinaweza pia kuchunguza namna waandishi wa jinsia tofauti wanavyowasilisha ujenzi wa uanaume, mamlaka ya kibabedume na gharama zinazowakabili wanaume. Utafiti wa aina hiyo utaendeleza mjadala kuhusu ubabedume katika fasihi ya Kiswahili na kusaidia kubainisha iwapo kinzani kati ya manufaa ya kijamii ya ubabedume na gharama zake kwa wanaume inajitokeza kwa namna inayofanana katika kazi mbalimbali za kifasihi.

**MAREJELEO**


Bertoncini-Zúbková, E. (Ed.). (1996). *Vamps and victims: Women in modern Swahili literature*. Rüdiger Köppe Verlag.

Connell, R. W. (1995). *Masculinities*. University of California Press.

Connell, R. W., & Messerschmidt, J. W. (2005). Hegemonic masculinity: Rethinking the concept. *Gender & Society, 19*(6), 829–859. https://doi.org/10.1177/0891243205278639

Courtenay, W. H. (2000). Constructions of masculinity and their influence on men's well-being: A theory of gender and health. *Social Science & Medicine, 50*(10), 1385–1401. https://doi.org/10.1016/S0277-9536(99)00390-1

Creswell, J. W., & Creswell, J. D. (2018). *Research design: Qualitative, quantitative, and mixed methods approaches* (5th ed.). Sage.

Ezeugwu, C. R., & Ojedokun, O. (2020). Masculine norms and mental health of African men: What can psychology do? *Heliyon, 6*(12). https://doi.org/10.1016/j.heliyon.2020.e05650

hooks, b. (2014). *Feminist theory: From margin to center*. Routledge. https://www.taylorfrancis.com/books/9781317588344

Janvan, P. W. (2023). *Ukandamizaji wa jinsia ya kiume katika riwaya teule za Kiswahili: Njozi Yapata Mtenzi (Mbatiah: 2018) na Nguu Za Jadi (Momanyi: 2019)*. University of Nairobi. https://erepository.uonbi.ac.ke/items/853c2f19-1744-40d6-af3c-7da0bbbe8045

Kiema, A. M., Mutua, J., & Ngesu, S. N. (2025). Changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume katika riwaya ya Nguu Za Jadi. *International Journal of Advance Research and Innovative Ideas in Education, 11*(4), 526–530. https://ijariie.com/manuscript/27069

Kimmel, M. S. (2008). *Guyland: The perilous world where boys become men*. Harper.

Kothari, C. R. (2004). *Research methodology: Methods and techniques* (2nd ed.). New Age International.

Kweyu, D. A. (2007). *A critical analysis of patriarchy and masculinity in Kezilahabi's Rosa Mistika and Kichwamaji*. University of Nairobi. https://erepository.uonbi.ac.ke/items/f74fc573-d8f4-405b-a352-f0ff72e7af2a

Lerner, G. (1986). *The creation of patriarchy*. Oxford University Press.

Manyanza, A. (2017). *Penzi la Damu*. E.A.E.P.

Maulid, H. M. (2025). Viashiria vya matatizo ya afya ya akili katika maisha ya ndoa kwa kuzingatia Nadharia ya Saiko-Changanuzi: Mifano kutoka riwaya ya Mungu Hakopeshwi na Penzi la Damu. *Abdulrahman Al-Sumait University Journal, 10*(2). https://doi.org/10.63104/suj.v10.i2.128

Messner, M. A. (1997). *Politics of masculinities: Men in movements*. Sage.

Millett, K. (1970). *Sexual politics*. Doubleday.

Momanyi, C. (2019). *Nguu za Jadi*. Queenex Publishers.

O'Neil, J. M. (2008). Summarizing 25 years of research on men's gender role conflict using the Gender Role Conflict Scale: New research paradigms and clinical implications. *The Counseling Psychologist, 36*(3), 358–445. https://doi.org/10.1177/0011000008317057

Onyango, J. O. (2007). Masculinities in Kiswahili children's literature in Kenya. *Swahili Forum, 14*, 245–254. https://d-nb.info/1238077781/34

Onyango, J. O., & Musa, Y. S. (2016). The portrayal of masculinities in a Kiswahili novel: The case of Nyota ya Rehema. *Islamic University Journal*, *4*(2). https://doi.org/10.4018/978-1-5225-0148-0.CH028

Osore, M. (2015). Femininity and masculinity in the novels of Euphrase Kezilahabi and Said Ahmed Mohamed. *Kioo cha Lugha*, *13*, 13–31. https://ir-library.ku.ac.ke/items/bf9d49bc-cedb-4c04-9a0f-0c79720b1507

Pleck, J. H. (1995). The gender role strain paradigm: An update. In R. F. Levant & W. S. Pollack (Eds.), *A new psychology of men* (pp. 11–32). Basic Books.

Silberschmidt, M. (2001). Disempowerment of men in rural and urban East Africa: Implications for male identity and sexual behavior. *World Development, 29*(4), 657–671. https://doi.org/10.1016/S0305-750X(00)00122-4

Stoebenau, K., Bingenheimer, J. B., Kyegombe, N., Datar, R., & Ddumba-Nyanzi, I. (2023). Development of the Gender Roles and Male Provision Expectations Scale. *Archives of Sexual Behavior, 52*, 2547–2564. https://doi.org/10.1007/s10508-022-02479-1

Topan, F. (2004). From Mwana Kupona to Mwavita: Representations of female status in Swahili literature. In P. Caplan & F. Topan (Eds.), *Swahili modernities: Culture, politics and identity on the East Coast of Africa* (pp. 213–227). Africa World Press.

Walby, S. (1990). *Theorizing patriarchy*. Basil Blackwell.